# DOYEN PUBLISHERS
## KENYA JUNIOR SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT
## MTIHANI WA MUHULA WA 1 2025
## GREDI YA 9 – KISWAHILI
*(Kartasi ya 2 - Insha na Utangulizi wa Fasihi)*

**Muda: Saa 1 dakika 45**

JINA: ______________________________________________

SHULE: ______________________________________________

KITENGO: ____________________ TAREHE: ______________________

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

a) Andika jina lako, shule, kitengo na tarehe katika sehemu zilizo hapo juu.
b) Karatasi hii ina sehemu mbili; **A** na **B**.
c) Jibu maswali **yote**.
d) Andika majibu **yote** kwa nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki.
e) Majibu **yote** ni lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

**RUBRIKI YA TATHMINI**

| ALAMA (%) | NGAZI |
|---|---|
| **80 - 100** | Anazidi matarajio |
| **60 - 79** | Anafikia matarajio |
| **40 - 59** | Anakaribia matarajio |
| **0 - 39** | Chini ya matarajio |

**ALAMA ZA MWANAFUNZI**

| ALAMA | | JUMLA |
|---|---|---|
| Sehemu ya A (Kutoka kwa 15) | | |
| Sehemu ya B (Kutoka kwa 35) | | |

***Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa. Watahiniwa wanapaswa kukagua karatasi hii ili kuhakikisha kuwa kurasa zote zimepigwa chapa kama ilivyosemwa na hakuna maswali yanayokosekana.***

## **SEHEMU A** (Alama 15)

**INSHA**

**Maagizo:**

a) Chukua muda wa dakika **40** katika zoezi hili.
b) Andika insha yenye maneno kati ya **300 - 350** katika nafasi uliyoachiwa.

1. *Rafiki yako amekuandikia barua kukujulia hali na kukuuliza mambo yanayohusiana na masuala ya masomo. Mwandikie barua kuijibu barua yake. Hakikisha kuwa unazingatia muundo wa kujibu barua ya kirafiki, ujumbe na lugha ifaayo.*

## **SEHEMU B** (Alama 35)

**FASIHI SIMULIZI (Alama 10)**

2. ***Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Ilikuwa alfajiri yenye baridi. Umande ulitapakaa kote. Ukungu ulitanda hivi kwamba hungeweza kumuona mtu alikuwa hatua chache mbele yako. Ndovu alipoamka, alikuta fisi mlangoni pake. Fisi alikuwa amemlimia ndovu shamba lake, lakini alikuwa hajalipwa ujira wake.

Kila alipomwendea ndovu kwa ajili ya malipo yake, fisi alitiliwa huku na kutolewa kule."Leo ni leo",fisi alimwambia ndovu."Nimevumilia vya kutosha. Kila siku ninapokuja kuchukua pesa zangu, hukosi hadithi mpya ya kunisimulia. Leo sitoki hapa bila pesa zangu!"

Fisi alipomaliza kumwaga joto lake, ndovu alimwambia: "Sikiliza fisi. Mimi nimeheshimika kote kijijini. Naona haja yako ni kunivunjia heshima –mbele ya familia yangu na wanakijiji kwa jumla. Sikulipi pesa zako, mpaka ujifunze kuwaheshimu wazee. Nakuamuru uondoke hapa mara moja, kabla sijakasirika! Nataka uende popote, unapofikiria kwamba unaweza kupata msaada. Ukienda kwa chifu, usisahau kwamba tunakunywa na yeye. Ukienda polisi, mkuu wa kituo amejaa tele mfukoni mwangu. Ukienda mahakamani, hakimu tulisoma darasa moja. Popote uendapo, hakuna yeyote atakayekusikiliza"

"Zaidi ya hayo, hakuna yeyote atakayekuamini.Mimi naitwa Bwana pesa.Kwangu umeota mpesapesa na kustawi. Nani ataamini kwamba naweza kushindwa kulipa vijisenti vichache ninavyodaiwa na fisi?"

Fisi alisikiliza kwa makini majitapo ya ndovu. Aliamua kumpasulia ndovu mbarika: "Bwana ndovu najua kuwa wewe una nguvu na uwezo mkubwa wa kifedha.Lakini hayo yote mimi hayanihusu ni yako na familia yako. Sitakuruhusu unidhulumu kilicho haki yangu. Usiutumie uwezo uliopewa na Muumba kuwaonea na kuwanyanyasa maskini wasio mbele wala nyuma" alimaliza usemi wake na kuondoka huku machozi yakimdondoka.

Fisi alipofika nyumbani, aliwasimulia fisi wanyonge wenzake yaliyomsibu.Fisi walikusanyika na kulizingira boma la ndovu huku wakisema: "Tunataka haki itekelezwe! Dhuluma lazima ikome! Unyanyasaji lazima ukome!" Ndovu aliposikia kelele langoni mwake, alipiga simu kwenye kituo cha polisi.

Mara, kikosi cha polisi wa kupambana na ghasi kiliwasili. Fisi walipigwa mijeledi na kuezekwa marungu. Waliojifanya mabingwa walipigwa risasi. Fisi waliosalia walikimbilia makwao, huku wakichechemea kwa maumivu. Mpaka wa leo fisi wangali wanatembea kwa kuchechemea.

a) Hadithi hii ina ujumbe gani kuu kuhusu heshima na haki? (alama 2)

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

b) Eleza sifa **mbili** za ndovu katika hadith hii. (alama 2)

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

c) Hadithi hii ni **hurafa** kwa sababu wahusika ni wanyama. Bainisha aina zingine **mbili** za hadithi. (alama 2)

d) Je, hadithi zina umuhimu gani katika jamii? (alama 4)

**NOVELA (Alama 10)**

3. ***Soma sehemu ifuatayo ya novela "Mshale wa Matumaini" na John Habwe kisha ujibu maswali.***

Mama yangu alikuwa miongoni mwa wanawake jasiri niliowafahamu wakati huo nikiwa mdogo. Alikuwa mkakamavu kuwashinda hata baadhi ya wanaume pale mtaani. Alipozungumza, alikuwa na hakika na alichokisema kila wakati. Nilimwona kuwa na busara nyingi. Alijiamini. Wanawake wengine walimsikiliza na kumwamini. Hata baadhi ya wanaume hali kadhalika. Baba alikuwa kinyume chake. Kila mara mama hakukoma kumkosoa na kumwelekeza baba kila ilipofaa.

Ilikuwa vigumu kuelewa tabia ya baba. Kuna wakati angekuwa mpole na wakati mwingine akawa mkali kupita kiasi. Nyumbani kwetu kulijulikana kama kwa mama Zahara kutokana na kujulikana sana kwa mama yangu na uhusiano mzuri aliokuwa nao na watu.

"Unajuaje kama habari hizi si kweli? Kwani huoni jinsi nyinyi Wareba mnavyotukandamiza kila mahali? Si uongozi, si biashara, hata kazi zote nzuri na zenye mishahara mizuri mnazifanya nyinyi. Sisi mmetuachia kazi zisizotamanika wala kutazamika. Lazima tuwe na haki sawa. Nyinyi Wareba mnatuonea sana," baba alimlalamikia mama siku moja.

Kutokana na uchache wa miaka yangu siku hizo, sikung'amua ni kitu gani kilichokuwa kikiendelea. Hata hivyo, licha ya utoto wangu, niling'amua kwamba baba yangu alikuwa akijipendelea sana na alikuwa mwingi wa ubinafsi; tabia ambayo mama yangu aliichukia na kuipinga kwa jino na ukucha.

a) Taja sifa **nne** za mama. (alama 4)

b) Ni maudhui yepi yanayojitokeza katika dondoo hili? (alama 2)

c) Eleza mbinu **moja** ya lugha ilizotumiwa katika sehemu hii ya novela. (alama 2)

d) Eleza sifa **moja** ya Wareba. (alama 2)

**TAMTHILIA (Alama 10)**

4. ***Jibu maswali haya kuhusu tamthilia.***

a) Eleza maana ya tamthilia. (alama 1)

b) Taja sifa **mbili** za tamthilia. (alama 2)

c) Tamthilia huwa na maelekezo ya jukwaani amabayo huandikwa kwa italiki. Maelekezo haya huelezea nini katika tamthilia? (alama 2)

d) Maudhui ni nini katika tamthilia? (alama 2)

e) Taja sifa **tatu** ambazo wahusika katika tamthilia wanaweza kuwa nazo. (alama 3)

**USHAIRI (Alama 5)**

5. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Wenye vyao watubana, twaumia maskini,
La kufanyiza hatuna, hali zetu taabani,
Kwa sasa kilo ya dona, bei mia ishirini,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

Washindana matajiri, kwa bei siyo utani,
Na pigo kwa mafakiri, tunao hali ya chini,
Wazeni kutafakari, wanyonge tu madhilani,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

Limekuwa kubwa zogo, hakwendeki madukani,
Fungu moja la muhogo, sasa shilingi miteni,
Huo mkubwa mzigo, waelemea vichwani,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

Si hichi wala si kile, hakuna cha afueni,
Bei imekuwa ndwele, wenye macho lioneni,
Ukiutaka mchele, pesa jaza mfukoni,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

Waliko hao samaki, huko ndiko uchawini,
Wachuuzi hawacheki, zimewatoka huzuni,
Vibuwa havishikiki, kimoja kwa hamsini,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

Maisha yetu viumbe, yamekuwa hilakini,
Wenye vyao kila pembe, wametukaa shingoni,
Nyama ya mbuzi na ng'ombe, sasa hali maskini,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

Maji yamezidi unga, kwa lodi wa darajani,
Kajitolea muhanga, kwa bei hawezekani,
Mvao wake wa kanga, ni shilingi elifeni,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 1)

______________________________________________

______________________________________________

b) Shairi hili lina beti ngapi? (alama 1)

______________________________________________

______________________________________________

c) Shairi hili ni la aina gani? (alama 1)

______________________________________________

______________________________________________

d) Bainisha kibwagizo cha shairi hili. (alama 1)

______________________________________________

______________________________________________

e) Eleza maana ya neno "**zogo**" kama lilivyotumika kwenye shairi. (alama 1)

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**